# HALMASHAURI YA WILAYA YA LIWALE

## MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI KILICHOFANYIKA TAREHE 04.02.2022 KWENYE OFISI YA ARIDH NA MALIASILI

**WALIOHUDHURIA**

1. Ndugu Damas M. Mumwi -Mkuu wa Idara ya Ardhi na Maliasili -Mwenyekiti
2. Ndugu Saturninus S. Mchallo -Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi -Katibu
3. Ndugu Bernard H. Kivamba -Mkuu wa Idara ya Mifugo na Uvuvi -Mjumbe
4. Ndugu Mustapha S. Magembe -Mkuu wa Idara ya Kilimo na Ushirika -Mjumbe

**WAALIKWA**

1. Ndugu Barikiel S. Sindato -Mwanasheria -Mshauri
2. Mhandisi R. Kazimoto - Mhandisi wa Umwagiliaji

**SEKRETARIETI**

1. 1. Ndugu Musa Malando -PMU
2. Ndugu Lucas Yusuph -PMU
3. Ndugu Sultani H. Ngojwike -PMU
4. Ndugu Somoe Kilwanda -PMU
5. Ndugu Zawadi Kimbendela-PMU
6. Ndugu Mariamu Mkambe -Mwandishi wa Mikutano

**WASIOHUDHURIA**

1. Dkt Gloria C. Andrew - Kwa taarifa

**Dondoo Na. 1 /Zabuni/2022 : KUFUNGUA KIKAO**

Katibu alimkaribisha Mwenyekiti ili afungue kikao baada ya kuona akidi ya wajumbe imetimia. Mwenyekiti alieleza kuwa kikao hicho ni cha kawaida cha kujadili taarifa mbalimbali hivyo wajadili kwa makini kwa manufaa ya Halmashauri.Baada ya maelezo hayo Mwenyekiti alifungua kikao saa 10:00 jioni

**Dondoo Na. 2/Zabuni/2022: KUTHIBITISHA AGENDA**

Yalifanyika marekebisho katika ajenda namba 9 baada ya kusomeka 'taarifa ya ujenzi wa josho la mifugo Kijiji cha Kimambi' isomeke 'taarifa ya ujenzi wa majosho ya mifugo Vijiji vya Kimambi, Luwele na Ndapata', baada ya marekebisho hayo Agenda za kikao zilithibitishwa.

**Dondoo Na 3/Zabuni/2022: KUSOMA NA KUTHIBITISHA MIHTASARI YA TAREHE 15/10/2021 NA 21/12/2021**

- **Muhtasari wa tarehe 15/10/2021**

Muhatasari wa kikao cha tarehe 15/10/2021ulisomwa ulithibitishwa na wajumbe kuwa kumbukumbu halali. Mwenyekiti na Katibu waliweka saini zao.



CamScanner

- **Muhtasari wa tarehe 21/12/2021**

Muhatasari wa kikao cha tarehe 21/12/2021ulisomwa ulithibitishwa na wajumbe kuwa kumbukumbu halali. Mwenyekiti na Katibu waliweka saini zao.

**Dondoo Na 4 /Zabuni/2022: YATOKANAYO NA MIHTASARI YA TAREHE 15/10/2021 NA TAREHE 21/12/2021**

Majibu ya utekelezaji wa maazimio hayo ya vikao vyote viwili yalisomwa na kupokelewa na wajumbe.

Katika kujadili ajenda hiyo katika azimio namba 1 la ukandarasi wa kujaza kifusi na kushindilia eneo la ukubwa wa Qubic mita $350m^2$ Stendi ya mabasi Liwale wajumbe waliweka mapendekezo kuwa Halmashauri itoe tangazo la kutoruhusu malori yenye uzito mkubwa kutoingia ndani ya Stendi hiyo ili maeneo hayo yasiharibiwe. Wajumbe walisem ni magari ya uziro wa Tani 10 tu ndiyo yanayotakiwa kuingia Stendi ya mabasi Liwale.

Katika azimio namba 2 la taarifa ya tangazo la zabuni ya ujenzi wa jengo la dharura Hospitali mpya ya Wilaya na jengo la Mtumishi kituo cha Afya Mpengere wajumbe walisisitiza kuwa Mhandisi wa Ujenzi na Kaimu Mkuu wa Idara ya Afya kuendelea kufuatilia Au kuandaa BOQ itakayotekelezwa kwenye miradi hiyo kwa njia ya 'Force Akaunti' . Wajumbe walilisema ujenzi huo uanze mara BOQ zitakapokuwa tayari na kuidhinishwa Mkkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Liwale

Ushauri ulipokelewa.

**Dondoo Na 5/Zabuni/2022: KUPOKEA TAARIFA YA TATHMINI YA TENDA YA UJENZI WA JENGO LA DHARURA HOSPITALI MPYA YA WILAYA NA JENGO LA MTUMISHI KITUO CHA AFYA MPENGERE.**

Katibu wa kikao aliwasilisha taarifa ya timu ya tathimini ya tenda ya ukandarasi wa ujenzi wa jengo la dharura eneo la Hospitali mpya ya Wilaya ya Liwale pamoja na tathimini ya jengo la Mtumishi Three in one katika kituo cha Afya Mpengere kama ifuatavyo;

1.Baada ya tathimini ya awali na ya kina , timu ya tathimini ilimhidhinisha Mkandarasi M/s Singilimo Enterprises Ltd wa sanduku la barua 45905 Dar es Salaam kujenga Jengo la Dharura Hospitali mpya ya Wilaya ya Liwale kwa mkataba wa shilingi Mia tatu Hamsini Milioni bila senti. (Tsh350,000,000.00) muda wa kumaliza kazi ni miezi sita (6) kuanzia siku ya kusainiwa mkataba

2. Baada ya tathimini ya awali na ya kina , timu ya tathimini ilimhidhinisha Mkandarasi M/s Liwale Construction Co. Ltd wa sanduku la barua 84 Liwale kujenga Jengo la mtumishi Three in one Kituo cha Afya Mpengere kwa mkataba wa shilingi Mia Moja Hamsini Milioni bila senti. (Tsh150,000,000.00) muda wa kumaliza kazi ni miezi sita (6) kuanzia siku ya kusainiwa mkataba

**Maoni ya PMU**

PMU walipitia kwa kina taarifa ya timu ya tathimini na kukubaliana nayo. Hata hivyo PMU inashauri Bodi ya zabuni kusitisha kazi hii kwa sababu bajeti iliyotengwa kukamilisha kazi hiyo kwa njia ya Mkandarasi ni ndogo kuliko inavyonekana baada ya BOQ za Wakandarasi.

| NA | JINA LA MRADI | MAKISIO/BAJETI | BAJETI YA MKANDARASI | MAONI YA PMU |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Jengo la Dharura Hospitali mpya ya Wilaya ya Liwale | 300,000,000.00 | 350,000,000.00 | Bajeti ya utekelezaji |
| 2 | Jengo la mtumishi Three in one Kituo cha Afya Mpengere | 90,000,000.00 | 150,000,000.00 | Bajeti ya utekelezaji |



CamScanner

- Katibu wa kikao alitoa taarifa ya kusitishwa kwa kazi ya ujenzi huo kwa njia ya Mkandarasi. Badala yake kazi hiyo imeelekezwa kufanyika kwa njia ya ''Force Account'' kwa bajeti ile ile 300,000,000.00 kwa jengo la dharura na Tsh. 90,000,000.00 kwa jengo la Mtumishi- Three in one
- Wajumbe wa bodi ya zabuni walikubalia na maoni ya PMU. Aidha wajumbe walipokea taarifa ya utekelezaji wa miradi hiyo kwa njia ya 'Force Akaunti' wakapendekeza PMU wakipokea BOQ ya utekelezaji wa ujenzi huo kwa njia ya 'Force Akaunti'taratibu ziendelee bila kuchelewa

**Dondoo Na 6/Zabuni/2022: KUIDHINISHA TANGAZO LA UJENZI NA UENDESHAJI WA MABANDA YA BIASHARA KUZUNGUKA UWANJA WA MICHEZO WA WILAYA YA LIWALE.**

Katibu aliwasilisha Tangazo la ujenzi na uendeshaji wa vibanda vya biashara kuzunguka uwanja wa michezo wa Halmashauri ya Wilaya ya Liwale. Wajumbe walichambua tangazo hilo kwa kina na kulifanyia maboresho kisha kuidhinisha tangazo la ujenzi na uendeshaji wa vibanda vya biashara kuzunguka uwanja wa michezo wa Wilaya ya Liwale. Wajumbe walishauri Tangazo litangazwe baada ya BOQ na michoro ya ujenzi kukamilika na kuidhinishwa na mamlaka.

**Dondoo Na 7/Zabuni/2022: TAARIFA YA KUPOKEA FEDHA SHILINGI 300,000,000.00 KWA AJILI YA MWENDELEZO WA UJENZI WA MAJENGO 5 YA HOSPITALI MPYA YA WILAYA.**

Katibu wa kikao alitoa taarifa ya kupokelewa kwa fedha shilingi 300,000,000.00 kwa ajili ya kumalizia jengo la Wadi ya Wazazi, jengo la Dawa, jengo la Kufulia, jengo la Mionzi na jengo la Utawala katika Hospitali mpya ya Wilaya ya Liwale. Kazi hiyo inatekelezwa kwa njia ya ''Force Account'' na kila jengo lina Fundi wake.

Wajumbe walipokea taarifa hiyo na kuidhinisha kazi hiyo iendelee kwa njia ya ''Force Account'' kama ilivyokusudiwa.

**Dondoo Na 8/Zabuni/2022: KUIDHINISHA UJENZI WA JENGO LA OPD , MAABARA,WAZAZI NA UPASUAJI KATIKA KITUO CHA AFYA MIRUI**

Katibu wa kikao alitoa taarifa kuwa Kituo cha Afya Mirui kimetengewa shilingi 450,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa majengo manne awamu ya kwanza kama ifuatavy:

1. Jengo la Wagonjwa wa nje OPD
2. Jengo la Wazazi lililoungana na jengo la Upasuaji
3. Jengo la maabara

Ilielezwa kuwa mradi huo utatekelezwa kwa njia ya ''Force Account'' . Wajumbe walipokea taarifa hiyo na kuidhinisha njia ya ''Force Account'' itumike kutekeleza ujenzi huo. Pili wajumbe waliazimia mradi huo uanze baada ya michoro na BOQ kuidhinishwa na kupokelewa PMU

**Dondoo Na 9/Zabuni/2022: TAARIFA YA UJENZI WA MAJOSHO YA MIFUGO KATIKA VIJIJI VYA KIMAMBI, LUWELE NA NDAPATA.**

Mhandisi wa Umwagiliaji aliwasilisha taarifa ya ujenzi wa majosho matatu (3) katika Halmashauri ya Liwale. Wizara ya Mifugo na Uvuvi inagharamia shilingi 18,000,000.00 kwa kila kijiji. Vijiji vitakavyonufaika na ujenzi huo ni KIMAMBI, LUWELE na NDAPATA



CamScanner

Mhandisi wa Umwagiliaji aliwasilisha BOQ ya makisio ya ujenzi wa Majosho sh. 105,000,000.00 kwa majosho matatu. Taarifa ilitolewa kuwa Halmashauri inatakiwa kuchangia sh. 16,000,000.00 na jamii ya wafugaji kwenye vijiji hivyo ichangie fedha iliyobaki kwa mujibu wa BOQ inayotekelezwa. Tazama Jedwali hapo chini ;

| NO | WACHANGIAJI WA FEDHA | KIASI KINACHOCHANGIWA |
|---|---|---|
| 1 | Wizara ya Mifugo na Uvuvi | 54,000,000.00 |
| 2 | Halmashauri | 16,000,000.00 |
| 3 | Jamii ya Wafugaji {Ndapata, Kimambi, & Luwele} | 35,000,000.00 |
| | **MAKISO YA MHANDISI** | **105,000,000.00** |

Taarifa ilipokelewa, Wajumbe wa Bodi ya zabuni walishauri Halmashauri ihamasishe jamii ya wafugaji kuchangia ujenzi wa Josho kwenye maeneo yao.

**Dondoo Na 10/ Zabuni/2022: MENGINEYO**

Wajumbe walimtaka Katibu wa kikao kufuatilia posho za wajumbe za vikao mbalimbali ambavyo hawajalipwa.

**Dondoo Na 11/ Zabuni/2022: KUFUNGA KIKAO**

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa majadiliano yao na alifunga kikao saa 12:25 jioni.

..........................................................

MWENYEKITI

KATIBU

TAREHE 22/4/2022

## YATOKANAYO NA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI CHA TAREHE 04.02.2022

| NA | AZIMIO | MHUSIKA | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| 1 | **Dondoo Na 4 /Zabuni/2022: YATOKANAYO NA MIHTASARI YA TAREHE 15/10/2021 NA TAREHE 21/12/2021**<br>BOQ ya 'Force Akaunti' ya ujenzi wa Jengo la Dharura Hospitali mpya ya Wilaya na Jengo la Mtumishi katika kituo cha Afya Mpengere ipatikane na ujenzi uanze | **HPMU & DMO** | Azimio limezingatiwa na za ujenzi zimeanza |
| 2 | **Dondoo Na 6/Zabuni/2022: KUIDHINISHA TANGAZO LA UJENZI NA UENDESHAJI WA MABANDA YA BIASHARA KUZUNGUKA UWANJA WA MICHEZO WA WILAYA YA LIWALE.**<br>Tangazo libandikwe baada ya BOQ na michoro ya ujenzi kukamilika. | HPMU | Tangazo lilikamilika kama ilivyoazimiwa. Hata hivyo halikubandikwa kwa sababu zoezi lilisitishwa na kikao cha Baraza la Madiwani la tarehe 8 & 9 Februari 2022 |